# MAELEZO MACHACHE YA LUGHA NA MASWALI

## SALAMU NA MAAMKUZI

| Salamu | Jibu | Wakati |
|---|---|---|
| Shikamoo | Marahaba | Wowote |
| Umeamkaje | Salama | Asubuhi |
| Asalaam aleikum | Aleikum salaam | wowote |
| Lala unono | Nawe pia | Usiku |
| Alamsiki | Binuru | Usiku |
| Ndoto njema | Nawe pia | Usiku |
| Mwambaje? | Sina la kuamba | Wowote |
| Tuonane kesho | Inshellah / Mungu akipenda | Usiku |
| Buriani | Buriani dawa | Kuachana |
| Sabalkheri | Akheri/ sabalkheri | Asubuhi |
| Masalkheri | Akheri/ masalkheri | Jioni |
| Makiwa | Tunayo/ yashapita | Matanga |
| Pole | Nishapoa | Wowote |
| Kwaheri | Yakuonana | Kuachana |
| Chewa | Chewa | Asubuhi |
| Karibu tule | Starehe | Wa kula |
| Hongera | Asante | Wowote |

## MASWALI

1. Mkikutana na mtu anayekuzidi umri utakuwa wa kwanza kumsalimia?
2. Jibu la "binuru" ni la salamu zipi?
3. Masalkheri ni salamu za wakati gani?
4. Watu walimkaribisha Maranga "Karibu tule"je, alijibuje?
5. Ungefika kwenye maziko ya hayati Jomo Kenyatta, ungewaombolezaji?

## NGELI

- Ngeli ni neno linalotumiwa katika sarufi ya Kiswahili kumaanisha mgawanyo wa nomino katika makundi. Ngeli huainishwa kwa msingi wa viambishi vitumiwavyo.

## MPANGILIO WA NGELI

### (i) A - WA

- Ngeli hii hurejelea viumbe wenye uhai kwa mfano: binadamu, samaki, ndege, wanyama na wadudu.
- Huchukua viambishi ngeli "a"katika umoja na "wa' katika wingi tunapotumia pamoja na vitenzi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mtu | Watu |
| 2. Punda | Punda |
| 3. Mnyama | Wanyama |
| 4. Ndege | Ndege |
| 5. Mdudu | Wadudu |
| 6. Mbwa | Mbwa |
| 7. Ng'ombe | Ng'ombe |
| 8. Mbu | Mbu |
| 9. Simba | Simba |
| 10. Nzi | Nzi |
| 11. Kuku | Kuku |
| 12. Samaki | Samaki |

## ZOEZI

**Geuza sentensi zifuatazo katika umoja**

1. Ndovu hawa ni wanene sana.
2. Ni wanyama wapi walioharibu mimea?
3. Mbwa wetu sio wenu.
4. Akina mama zetu wamefika salama?
5. Ndege wengi ni wale wanaoruka angani.

### (ii) KI – VI

- Huchukua viambishi ngeli "ki" katika umoja na "vi" katika wingi tunapotumia pamoja na vitenzi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kidonda | Vidonda |
| 2. Kiambaza | Viambaza |
| 3. Kiti | Viti |
| 4. Kituo | Vituo |
| 5. Kitanda | Vitanda |
| 6. Kinanda | Vinanda |
| 7. Kikapu | Vikapu |
| 8. Chama | Vyama |
| 9. Kikundi | Vikundi |
| 10. Chakula | Vyakula |
| 11. Kisiwa | Visiwa |
| 12. Cheo | Vyeo |
| 13. Kinywaji | Vinywaji |
| 14. Choo | Vyoo |
| 15. Chombo | Vyombo |
| 16. Chungu | Vyungu |

## ZOEZI

**Badilisha sentensi hizi katika wingi**

1. Choo hiki ni chake.
2. Chombo chako kimebingirikabingirika.
3. Chama chake kilisambaratika.
4. Kichaka kile kirefu kina simba wengi.
5. Kiini kinachosababisha UKIMWI kimejulikana.

### (iii) LI – YA

- Huchukua viambishi ngeli "ma"katika wingi tunapotumia pamoja na vitenzi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Gari | Magari |
| 2. Jitu | Majitu |
| 3. Gunia | Magunia |
| 4. Jikalamu | Majikalamu |
| 5. Jiwe | Mawe |
| 6. Dawati | Madawati |
| 7. Jino | Meno |
| 8. Gurudumu | Magurudumu |
| 9. Jicho | Macho |
| 10. Embe | Maembe |
| 11. Jambo | Mambo |

| | |
|---|---|
| Chakula cha jioni | Chajio |
| Mtu asiye na kwao | Msikwao |
| Chakula cha mchana | Chamcha |
| Ujumbe mfupi wa rununu | Ufuru |
| Chakula cha kuamsha kinywa | Chamsha |
| Upungufu wa kinga mwilini | Ukimwi |

## VIVUMISHI

- Kivumishi ni neno linaloeleza habari za mtu, namna alivyo, au kitu jinsi kilivyo, jinsi kinavyoonekana au kinavyofikiriwa. Kivumishi hutokana na neno VUMA yaani kutoa au kueneza habari.

## AINA YA VIVUMISHI

**(i) Vivumishi vya sifa:**

- Hueleza hali ya kitu, urefu, ukubwa, ufupi, udogo, k.m

-eupe -eusi
-ekundu -dogo
-epesi -bovu
-geni -fupi

**(ii) Vivumishi vya idadi**

- Huonyesha idadi ya vitu mambo yanayorejelewa k.m

-wengi
-chache
-watatu
-manne
-khumusi

**(iii) Vivumishi vimilikishi:**

- Kumiliki ni kutamalaki. Kuwa mali ya mtu au watu fulani. Vivumishi vimilikishi huingia hali tatu ukitumia wingi wa hali hizo kulingana na ngeli tofauti.
- Vimilikishi hivi pia hutegemea sana nafsi tatu.

**-angu** (mimi) - **etu** (sisi) k.m
mtoto wangu - watoto wetu
**ako** (wewe) - **enu**(nyinyi) k.m
kitabu chako - vitabu vyenu
**ake** (yeye) - **ao** (wao) k.m
gari lake - magari yao

- Vimilikishi hivi hubadilika tu kulingana na viambishi ngeli katika umoja na wingi.

## MASWALI

**Geuza sentenzi zifuatazo kwa umoja**

1. Sisi sio nyinyi wala wao.
2. Vitabu vyenu vimeibiwa.
3. Ng'ombe wao wameuzwa .
4. Miti yetu itakatwa leo jioni.
5. Nyayo zenu zimedungwa na miiba.

**Vivumishi viashiria :**

- Kiashiria ni neno linaloonyesha mahali kitu kilipo au umbali wa kitu.
- Kulingana na ujirani wa kitu kingine. Viashiria pia huitwa VIONYESHI. Vinaweza kuwa karibu,karibu kiasi na mbali.

| | | | |
|---|---|---|---|
| A-WA | Huyu / hawa | Huyo / hao | Yule / wale |
| LI-YA | Hili / haya | Hilo / hayo | Lile / yale |
| KI-VI | Hiki / hivi | Hivi / hivyo | Kile / vile |
| I-ZI | Hii / hizi | Hiyo / hizo | Ile / zile |
| U-I | Huu / hii | Huo / hiyo | Ule / ile |
| U-ZI | Huu / hizi | Huo / hizo | Ule /zile |
| YA-YA | Haya | Hayo | Yale |
| U-YA | Huu / haya | Huo / hayo | Ule / yale |
| PA | Hapa | Hapo | Pale |
| KU | Huku | Huko | Kule |
| MU | Humu | Humo | Mle |

## VIVUMISHI VIASHIRIA RADIDI:

- Vivumishi hivi hurudiwa ili kutilia mkazo. Pia hubadilika kulingana na ngeli.

| | | | |
|---|---|---|---|
| A-WA | huyu huyu / hawa hawa | huyo huyo / hao hao | yule yule / wale wale |
| LI-YA | hili hili / haya haya | hilo hilo / hayo hayo | ile lile / yale yale |
| KI-VI | hiki hiki / hivi hivi | hicho hicho / hivyo hivyo | kile kile / vile vile |
| I-ZI | hii hii / hizi hizi | hiyo hiyo / hizo hizo | ile ile / zile zile |
| U-I | huu huu / hii hii | huo huo / hiyi hiyo | ule ule / ile ile |
| U-ZI | huu huu / hizi hizi | huo huo / hizo hizo | ule ule / zile zile |
| YA-YA | haya haya | hayo hayo | yale yale |
| U-YA | huu huu / haya haya | huo huo / hayo hayo | ule ule / yale yale |
| PA | hapa hapa | hapo hapo | pale pale |
| KU | huku huku | huko huko | kule kule |
| MU | humu humu | humo humo | mle mle |

## VIVUMISHI VIASHIRIA VISISITIZI.

- Hivi ni viashiria vya kusisitiza au kutilia mkazo zaidi. Visisitizi hivi huchukua mizizi haswa ya viambishi ngeli.

| | | | |
|---|---|---|---|
| A-WA | Yuyu huyu / wawa hawa | yuyo huyo / wao hao | yule yule / wale wale |
| LI-YA | lili hili /yaya haya | lilo hilo /yayo hayo | lile lile /yale yale |
| KI –VI | kiki hiki / vivi hivi | kicho hicho /vivyo hivyo | kile kile / vile vile |
| I-ZI | ii hii / zizi hizi | iyo hiyo / zizo hizo | ile ile /zile zile |
| U-I | uu huu / ii hii | uo huo / iyo hiyo | ule ule / ile ile |
| U–ZI | uu huu / zizi hizi | uo huo / zizo hizo | ule ule / zile zile |
| U-U | uu huu | uo huo | ule ule |
| YA-YA | yaya haya | yayo hayo | yale yale |

| | | | |
|---|---|---|---|
| KU | kuku huku | kuko huko | kule kule |
| PA | papa hapa | papo hapo | pale pale |
| MU | mumu humu | mumo humo | mle mle |

**MASWALI**

**Geuza viashiria radidi vifuatavyo viwe viashiria visisitizi.**

1. Mkoba huu huu ulinunuliwa jana.
2. Kuimba huko huko kuliwafurahisha wageni.
3. Wakulima hawa hawa watanufaika na kilimo cha paleto.
4. Matunda yale yale yatapelekwa masokoni.
5. Vyeo hivyo hivyo walivyopandiswa vimefutiliwa mbali.
6. Kuta hizi hizi zilizobomoka zitajengwa upya.
7. Maziwa hayo hayo yameharibika.
8. Wanafunzi hawa hawa wameahidi kutia juhudi.
9. Ufisadi huo huo ulimtia taabani.
10. Miti hiyo hiyo itatumika katika ujenzi.

**ZOEZI**

**Badilisha sentensi hizi kwa umoja.**

1. Nyuzi zizi hizi ni zao.
2. Nyavu hizo hizo zimekatika .
3. Mikono hii hii imeumia nilipokuwa nikicheza voliboli.
4. Mawe yale yale yatatumiwa katika ujenzi.
5. Vidonda vivyo hivyo vitasababisha magojwa ya pepopunda.
6. Miembe hiyo hiyo itakatwa kesho asubuhi.
7. Nzi wao hao hueneza kipindupindu.
8. Mahali papa hapa patatumika katika michezo ya vikapu.
9. Ngozi zile zile ni za mamba.
10. Ajali zizo hizo zimesababisha vifo.

**VIVUMISHI VYA PEKEE**

**- INGINE:**

- Ni kivumishi chenye maana "sehemu ya / baadhi ya / zaidi ya" k.m

(a) Mtu mwingine ni huyu - watu wengine ni hawa.

(b) Gali jingine / lingine limenunuliwa - magari mengine yamenunuliwa.

(c) Mahali pengine ni pale n.k

**- INGINEO:**

- Hutumiwa kutoa maana ya "zaidi ya/dhana ya zaidi"k.m

(a) Kucheza kwingineko hakufai.

(b) Miti mingineyo itakatwa.

(c) Maji mengineyo hayatakikani.

**-O-OTE:**

- Ni kivumishi kinacholeta dhana ya "kutochagua / kutobagua / kutojali" k.m

(a) Shuleni kokote hakukosi walimu.

(b) Karatasi yoyote itafaa kuandika - karatasi zozote zitafa kuandika

(c) Mwalimu yeyote atafundisha - walimu wowote watafundisha.

(d) Gari lolote litakwama - magari yoyote yatakwama.

**-OTE:**

- Ni kivumishi kinachoonyesha kuhusika kwa jambo kwa wingi wake bila kupungua. Ote haichukui viambishi vya ngeli ya a-wa katika umoja. Mifano
  - Wanafunzi wote walifaulu.
  - Mti wote utakatwa - miti yote itakatwa.
  - Ukuta wote umebomoka - kuta zote zimebomoka.
  - Mahali pote pamejaa maji.

**ENYE:**

- Ni kivumishi kinachoonnyesha dhana ya" kuwa na/umilikisho wa mali, tabia, hali na cheo" k.m

(a) Jeff mwenye mali ni huyu - akina Jeff wenye mali ni hawa.

(b) Nguo yenye madoadoa hupendeza - nguo zenye madoadoa hupendeza.

(b) Kitabu chenye picha ni hiki - vitabu vyenye picha ni hivi.

**ENYEWE:**

- Ni kivumishi kinachotumiwa kuonyesha nafsi kwa kusudi la kusisitiza. Pia hutumika kuvumisha vitu visivyo na nafsi kwa ajili ya kutilia mkazo juu ya jambo linalojulikana kwa wanaoshiriki k.m

(a) Mwenyewe hayupo - wenyewe hawapo.

(b) Lete barua yenyewe - lete barua zenyewe.

(c) Mkate wenyewe umeoza - mikate yenyewe imeoza.

(d) Maziwa yenyewe yameharibika.

**MASWALI**

**Jaza vivumishi vya pekee vinavyofaa kwenye kifungu kifuatacho.**

Nchi ___1___amani hupata maendeleo. Wananchi ___2___wanafaa kuishi kwa amani, upendo na umoja. Watu ___3___lazima wathamini amani. Maendeleo ___4___hupatikana kulipo na amani. Viongozi___5___kuhubiri amani wanafaa kupongezwa. Kujuta ___6___hakufai ikiwa hatukuishi kwa amani. Katika nchi ___7___ tumeshuhudia vita vya ___8___ kwa___9___, watu ___10___wa mepoteza maisha. Ukitaka kujua uzuri wa mwangaza ingia gizani.

**MNYAMBULIKO WA VITENZI**

Kitenzi - Ni neno linaloeleza kitendo kinachofanywa wakati fulani. k.m

(i) Kaka anakata mti. a-na-kata;_kata ni kitenzi.

(ii) Sisi tunasoma Kiswahili.__tu - na_ soma;_soma ni kitenzi.

**Mnyambuliko wa vitenzi.**

- Ni mfano wa kuvibadilisha vitenzi katika hali

mbalimbali kwa kurefusha / kugeuza viambishi tamati. Kitenzi kimoja kinaweza kunyambuliwa k.v

**(i) KUFANYA**

- Hutumiwa kuonyesha uhusiano wa kitenzi na mtendaji ile hali ya kuwezesha jambo fulani, litoke. Kutenda kitu Na si lazima ijulikane ni kwa ajili ya nani k.m
  (i) Mwizi **alivunja** mlango.
  (ii) Msasi **hutega** wanyama.

**(ii) KUFANYIA**

- Hutuwezesha dhana ya kitenzi kilichotendwa kwa niaba ya / badala ya. Mara nyingi mnyabuliko huu wa vitenzi huishia na **"ia"** au **"ea"** k.m
  (i) Dada alinivulia nguo.
  (ii) Nilimsomea babu barua.
- Hutumiwa kueleza / kuonyesha kuweko Kwa mwendo kutoka Kwa kitu kimoja kuendea kingine k.m
  (i) Basi lilipokuwa likiondoka utingo alilirukia.

**(iii) KUFANYIKA**

- Kitu kutendeka bila nguvu za mtu yeyote. Aghalabu mnyambuliko huu wa vitenzi huishia na **"ka"** k.m
  (i) Mlango ulifungika.
  (ii) Maandishi yanasomeka.
  (iii) Maandishi yamefutika

**(iv) KUFANYIWA**

- Kitendo kinachofanywa na mtu mwingine Kwa kukutendea wewe ambaye hufanyi chochote.Pia vitenzi hivi huishia na **"wa"** Kufanya kwa niaba ya mtu mwingine k.m
  (i) **Alisomewa** barua.
  (ii) Kitabu **kiliandikiwa** wanafunzi.
  (iii) **Alipigiwa** simu na Rais.

**(v) FANYWA**

- Jambo Fulani kutendwa na sio lazima ijulikane ni kwa ajiliya nani / sababu gani, Vitenzi hivi pia huishia na silabi tatu **"–wa"** k.m
  (i) Barua **ilisomwa** na yeye.
  (ii) Kitabu **kitaandikwa** mwaka ujao.
  (iii) Nguo **zimepigwa** basi.

**(vi) FANYIANA**

- Kufanya kitu kwa ajili ya mwingine nawe pia kufanywa tendo hilo hilo, vitenzi husika huishia na **"iana / eana** k.m
  (i) **Waliandikiana** barua.
  (ii) **Walipigiana** simu.
  (iii) **Wamesameheana**

**(vii) FANYANA**

- Kitendo hiki kinafanywa na watu wawili au zaidi na hutendwa kwa wakati mmoja. Vitenzi huishia na **"na"** k.m
  (i) **Walipigana** mbele ya umati mkubwa.
  (ii) Walikuwa **wakipendana** kama chanda na pete.
  (iii) **Tulijulishana** habari muhimu.

**(viii) FANYISHA**

- Kulazimisha kitendo kufanywa , pia vitenzi huishia kwa **"sha / za / sa** k.m
  (i) Dawa za **kulevya** hudhuru afya.
  (ii) **Pangusa** mahali hapa.
  (iii) **Punguza** sauti ya redio.

**(ix) FANYISHWA**

- Kulazimishwa kutenda jambo , vitenzi huishia na:- **-wa"** k.m
  (i) Makundi hayo mawili yalipiganishwa.
  (ii) Viumbe vyote **viliumbwa** na Maulana
  (iii) Gari lile **liliundwa** likaundika. n.k

**(x) FANYAFANYA**

- Kurudiarudia jambo, kitenzi hurudiwaridiwa k.m
  (i) Kurandaranda ni tabia mbaya.
  (ii) Kusemasema mambo ya watu kutafanya watu kuzozana.
  (iii) Kupigapiga watoto ni kukiuka haki za watoto. n.k

## VIVUMISHI TASA

Ni maneno yasiyochukua viambishi ngeli, pia hayana umoja wala wingi k.m.

| | | |
|---|---|---|
| -hodari | -rahisi | -hatari |
| -saba | -sita | -haba |
| -tisa | -kumi | -tajiri |
| -bure | -maridadi | -madhubuti |
| -gani | -maalum | -rojorojo |
| -ghali | -dhaifu | -duni |
| -sanifu | -safi | -maridhawa |
| -laini | -nadhifu | -rahisi |
| -lufufu | -tele | -bora |
| -kamili | -stadi | -haramu |

**Mifano ya sentensi:**

(a) Mnawaita watoto gani?
(b) Vijana hodari walituzwa.
(c) Gari safi liliegeshwa.
(d) Msichana nadhifu anasoma.
(e) Vyakula bora viliiwa.

**ZOEZI**

**Pigilia vivumishi tasa msitari**

1. Mkulima huyo alivuna mavuno maridhawa.
2. Ni bora kuwa mwalimu kuliko daktari.
3. Nilipotuzwa nilibanwa na furaha tele.
4. Kufanya biashara haramu ni hatia.
5. Umefanya kazi duni kwa sababu wewe ni dhaifu.

## VIHISISHI / VIINGIZI

Kihisishi ni tamko la kuonyeshea hisia za ndani. Tutumiapo vihisishi kihisi '!' hutumika.Tuna vihisishi mbalimbali;

(a) Hisia za huzuni :- Pole! Ole wake!
(b) Woga:- Mungu wangu! Mama wee! Mtume simama! Toba!
(c) Huruma:- Maskini! Pole!
(d) Mshangao:- Lo! Ahaa! Oo! Salaale! Lakwata!

(e) Furaha:- Huree! Aha! Alhamdulillahi! Ewaa! Oyaa!
(f) Hasira:- Kha! Ah!
(g) Majuto:- Ole wangu! Laiti! Lau!
(h) Kukemea:- We! Ebo!
(i) Kukanusha / kukataa:- Ata! Hata! La hasha! Hasha lillahi!
(j) Kukubali:- Haya! Enhe! Naam! Ohoo! Hewala!
(k) Kiapo:- Haki ya Mungu! Wallahi! Tallahi! billahi!
(l) Fedheha:- Astsfullah!
(m) Heshima:- Allah! Allahualmu! Allahu akbar!
(n) Chuki:- Ebo! Usu! Fedhuli we! Kefle!

## VIWAKILISHI

Ni vibadala au maneno yanayotumiwa kuwakilisha nafsi ya mtu wa kwanza wa pili na watatu katika umoja na wingi. Pia huwakilisha majina mbalimbali katika ngeli zote.

(a) Viwakilishi vya nafsi ya kwanza.
- Mimi - ni * Mimi **ni** mwalimu katika shule hii.
- Sisi_-_tu * Sisi **tu** walimu katika shule hizi.

(b) Viwakilishi vya nafsi ya pili.
- Wewe_-_u * Wewe **u** mwanafunzi stadi.
- Nyinyi_-_mu * Nyinyi **mu** wanafunzi stadi.

(c) Viwakilishi vya nafsi ya tatu.
- Yeye_- a *Yeye ameenda kwake.
- Wao _-_wa *Wao wameenda kwao.

**Tambua viwakilishi.**
1. Kalamu hii ni yangu, ile ni yako.
2. Yeye hapeendi uzembe.
3. Hiki ni kitabu cha yule mwanafunzi.
4. Mwalimu huyo ni stadi, yeye pia ni mkulima.
5. Kikulacho ki nguoni mwako.

## NYAKATI

Tunazo nyakati mbalimbali ambazo huwakilishwa kwa viambishi mbalimbali kuashiria majira:
1. Wakati uliupo (wakati leo)_kiwakilishi "na" hutumika k.m.
   - Wanafunzi wanasoma.
   - Sisi tunasoma.
2. Wakati uliopita (wakati jana)_kiwakilishi "li" hutumika k.m,
   - Wanafunzi walisoma.
   - Tulivisoma vitabu vyote.
3. Wakati ujao (wakati kesho)_kiwakilishi "ta" hutumika k.m
   - Wanafunzi watasoma.
   - Tutavisoma vitabu vyote.
4. Wakati wa mazoea (kila wakati)_kiwakilishi "hu" hutumika k.m
   - Wanafunzi husoma.
   - Sisi huvisoma vitabu vyote.
5. Wakati timilifu (uliotimia) kiwakilishi "me" hutumika k.m
   - Wanafunzi wamesoma.
   - Tumevisoma vitabu vyote.
6. Wakati ujao hali ya kuendelea kwa kitendo_"takuwa na ki" hutumika k.m
   - Wanafunzi watakuwa wakisoma.
   - Tutakuwa tukisoma masomo yote.
7. Wakati uliopita hali ya kuendelea kwa kitendo"likuwa na li" hutumika k.m
   - Wanafunzi walikuwa wakisoma.
   - Tulikuwa tukisoma vitabu.
8. Wakati tegemezi kiwakilishi " nge na ngali" hutumika k.m angeniita ningeitika.

**TANBIHI: MATUMIZI YA "NGE NA NGALI"**
- Nge huandamana na nge kwenye sentensi k.m ningekuwa na pesa ningenunua gari. (sina pesa ndio mana sijanunua gari).
- Ngali huandamana na ngali kwenye sentensi k.m ningalikuwa na pesa ningalinunua gari. (sikununua gari kwa sababu sikuwa na pesa)
- Unapokanusha unatangulisha kiambishi "si" k.m _ningekuwa tajiri ningenunua gari—nisingekuwa tajiri nisingenunua gari(nilikuwa tajiri nikanunua gari).

**ZOEZI**

**Badilisha sentensi zifuatazo kulingana na maagizo kwenye mabanoni.**
1. Ukifanya bidii utafaulu (tumia nge)
2. Anapenda kuogelea (wakati wa mazoea)
3. Amefika Mombasa jana alfajili (wakati uliopita)
4. Nilipoenda kwake sikumpata (wakati ujao)
5. Watalima shamba lote leo (wakati uliopo)
6. Mngetuita tungeitika (kanusha)
7. Ningeenda kwao juzi ningempata( tumia ngali)
8. Wasingaliishi kwa amani wangalipigana (kanusha utumie nge)
9. Tungekula tungeshiba (eleza maana ya sentensi)
10. Usingalisoma kwa bidii usingalifaulu (eleza maana ya sentensi)

**MATUMIZI YA "KWA"**

(i) Hutumika kuonyeshea kuwa jambo au kitu fulani kilitumika kufanyia jambo fulani k.m
- Alinipiga kwa jiwe.
- Alisafiri kwa gari.
- Nilienda kwa miguu.

(ii) Kwa hutumika kuonyeshea kusudio au sababu, k.m
- Aliadhibiwa kwa kukosa adabu.
- Alifungwa jela kwa wizi wa mabavu.
- Alilia kwa kusikia uchungu.

(iii) Hutumika kuonyeshea jinsi jambo lilivyofanywa au litakavyofanywa k.m
- Aliingia kwa siri.
- Alilia kwa uchungu.
- Alitembea kwa maringo.

(iv) Hutumiwa pamoja na maneno ya sifa ambayo huonyesha umilikaji k.m

- Kwao ni mbali.
- Nitaenda kwangu leo jioni.
- Kwako ni karibu na kwake.

(v) Hutumiwa kuonyesha nia ya neno k.m
- Walifika wadogo kwa wakubwa.
- Tulikula wali kwa nyama.
- Wazee kwa vijana walivamiwa.

(vi) Kwa hutumiwa kuonyeshea mahali k.m
- Kwa Sibwoga ni Kibera.
- Tutaenda kwa Mwangangi keshokutwa.
- Kwa Juma ni karibu na kwetu.

(vii) Hutumiwa kuonyeshea sehemu moja au sehemu kadha za kitu kizima k.m
- 7/12 saba kwa kumi na mbili.

(viii) Hutumiwa kuonyesha kiunganifu 'a' cha ngeli ya 'ku'(vitenzi) k.m
- Kusoma kwa Gilbert ni kuzuri.
- Kuimba kwa Wanjala kunapendeza.

## MATUMIZI YA "KI"

1. Ki hutumika katika mwanzo wa ngeli ya ki-vi k.m kijiko-vijiko, Kitanda - Vitanda
2. Ki hutumika kuonyeshea sifa katika hali ya kufananisha k.m
   - Lameck alitembea kizee.
   - Monyoro alicheza kitoto.
3. Hutumika kuonyeshea udogo k.m
   - Kitoto hiki ni kizuri sana.
   - Kijikalamu changu kimepotea.
4. Hutumika katika mwanzo wa maneno yanayoonyesha lugha za watu fulani k.m
   - Kifaransa ni lugha rahisi kujifunza.
   - Mzee atatufundisha lugha ya Kimaasai.
5. Huonyeshea kitendo kinachoendelea wakati fulani k.m
   - Wanafunzi walikuwa wakiimba nilipofika.
   - Alikuwa akila nilipomwona.
6. Ki hutumika kuonyeshea masharti k.m
   - Ukisoma utafaulu.
   - Ukipanda pantosha utavuna pankwisha.
   - Ukija utanipata.

## MATUMIZI YA "NI"

1. Ni huwekwa mwishoni mwa kitenzi au kiarifa kuashiria wingi na kushurutisha k.m
   - Simama kule (umoja)_-_simameni kule (wingi)
   - Njoo hapa (umoja)_- njooni hapa (wingi)
2. Ni ikiwekwa mwishoni mwa nomino ya kitu nomino hiyo hubadirika na kuwa nomino ya mahali k.m
   - Nyumba (nomino/jina) -_nyumbani (mahali)
   - Shule ( nomino)_-_shuleni (mahali)
3. Ni ya nafsi – huashiria nafsi ya kwanza katika hali ya umoja k.m
   - Nitajitahidi zaidi.
   - Ninasoma kitabu cha hadithi.
4. Ni ya kiulizi k.m
   - Lini utaenda kwao?
   - Kalamu gani yako?
   - Nini kinachokusumbua?
   - Nani amefanya amemaliza kazi?
5. Ni ya kiunganishi k.m
   - Mwalimu Njoroge ni shujaa.
   - Kwa Ojwang ni Kabiria.

## MATUMIZI YA "NA"

1. Hutumika kama kiunganishi k.m
   - Sheilla na George ni ndugu wa toka nitoke.
   - Nairobi na Mombasa ni miji mikuu nchini.
2. Huonyeshea mazoea k.m
   - Ninapenda kusoma
3. Kuonyeshea umilikaji k.m
   - Nina kitu kizuri.
   - Otieno ana mali mengi.
4. Hutumika kuonyeshea kitendo kinachoendelea wakati uliopo k.m
   - Anasoma Kiswahili.
   - Anaimba wimbo wa taifa.
5. Hutumika kuonyeshea kitendo cha kufanyiana k.m
   - Wanasaidiana kazi.
   - Waliandikiana nyaraka.
6. Na hutumika badala ya neno "kama" k.m
   - Mtoto amefanana na babake

## MATUMIZI YA KARIBU

1. Karibu hutumika kuonyeshea masafa (umbali) k.m
   - Tunaishi karibu na soko.
   - Kwao ni karibu na mto Tana.
2. Karibu hutumika kati makaribisho k.m
   - Mwenyeji alijibu "karibu"
3. Hutumika kuonyeshea kitendo kukaribia kutendeka (karibu ya nusura) k.m
   - Karibu aibuke mshindi.
   - Alikuwa karibu kuzama.
4. Karibu ya kiasi (idadi) k.m
   - Alikula karibu chakula chote.

## MATUMIZI YA KATIKA

1. Hutumika kuonyeshea mahali fulani. Hutumiwa badala ya kiambishi ni k.m
   - Panya aliingia katika pango.
   - Ametoka katika nyumba.
   - Katika chuo hiki kuna dhulma ya hali ya juu.

**ONYO:** Huwezi kutumia katika na ni kwenye sentensi moja k.m panya aliingia katika pangoni.

2. Hutumika kuonyeshea hali (kitendo kinachofanyika) katika hali gani? k.m
   - Katika kufanya hivyo alikosea.
   - Katika kuruka kwake alivunjika mguu.
   - Yuko katika hali ya kukasirika.

**MATUMIZI YA JI**

1. Ji - ya nafsi – Mtendaji anapojirejelea k.m Nilijiuliza maswali mengi.
2. Ji - ya mtendaji – Huwekwa mwishoni mwa neno kuashiria anayetenda k.m Anayesoma ni msomaji.
3. Ji - ya Ukubwa – Huwekwa mwanzoni mwa baadhi ya nomino kuashiria ukubwa k.m jitu, jibwa n.k
4. Ji – ya kuonyesha hali – uogeleaji wake unavutia.

**MATUMIZI YA "PO"**

(i) Po - ya mahali.
Huongezwa mwishoni mwa kitenzi kuonyesha kitendo kilipofanyika k.m
- Ulalapo ni pale.
- Uchezapo watu hufurahi.
- Usomapo ni hapa.
- Uandikiapo pana uchafu.

(ii) Po - ya wakati.
Hutumika kuonyeshea kuwa kitendo fulani kilifanyika / kitafanyika na kufuatwa na kitendo kingine k.m
- Aliponitafuta alinipata shuleni.
- Mtakapojitahidi mtapita.
- Aliponiita niliitika.

**MATUMIZI ''LICHA YA''**

- Hutumiwa kuleta maana ''zaidi ya'' mbali na k.m
  - Licha ya kupoteza vitabu alichafua nguo zake kwa wino.
  - Utingo alining'inia kwenye gari licha ya kuonywa na polisi.
  - Hakuweza kupata alama ya 60 licha ya kufunzwa na mwalimu.

**MATUMIZI YA VILE**

- Hutumiwa kwa njia tatu.

1. Kivumishi kionyeshi (kiashiria) cha mbali katika ngeli ya ki-vi k.m
   - Kiti kile ni changu – Viti vile ni vyetu.
   - Vyandarua vile ni vizuri.
2. Hutumiwa kuleta maana ya namna au jinsi huonyesha kitendo kile kimefanyika katika] sentensi k.m
   - Alikula vile kwa sababu alikuwa na njaa.
   - Walishindwa vile kwa sababu ya kukosa mazoezi.
3. Hutumika kwa kurudiwarudiwa kuleta maana ya pia / tena k.m
   - Vilevile kulikuwa na ngoma za kitamaduni.
   - Vilevile Major Blue alitunukiwasifa nzuri.

**ZOEZI**

**Tofautisha sentensi hizi.**

1. Vilevile vikombe vilipasuka.
   - Vikombe vilevile vilipasuka.
   - Vikombe vilipasuka vilevile.
2. Alionyeshwa vile viti vya kutengenezwa – Kiashiria.
   - Alionyeshwa viti vile vya kutengenezwa - Namna.
   - Alionyeshwa viti vya kutengenezwa – Pia.

## MSEMO HALISI NA MSEMO WA TAARIFA

**MSEMO HALISI**

- Msemo halisi ni kauli ya maneno au matamshi yalivyosemwa na mzungumzaji. Maneno haya huhainishwa jinsi yalivyo bila kubadilisha chochote.
  - Alama za mtajo / nukuu hutumika katika usemi halisi kubainisha maneno ya msemaji.
  - Maneno ya msemaji katika usemi halisi baada ya koma lazima yaanze kwa herufi kubwa.
  - Nyakati zote zinaweza kutumiwa katika usemi halisi.
  - Mfano, Juma alisema, ''Nitaenda.''
  - Vibainishi kama akasema, akauliza , hutumiwa baada au kabla ya usemi halisi.
  - Kwa ujumla kanuni za kawaida za uakifishaji hutumiwa katika usemi halisi.

**USEMI WA TAARIFA**

- Huwa ni ripoti ya maneno yaliyosemwa na mtu mwingine na maneno halisi ya mnenaji hayatumiwi.
- Alama za mtajo hazitumiwi katika usemi taarifa.
- Vilevile alama za hisia hazitumiwi badala yake kuna maneno maalum yanayotumiwa kuleta zile hisia. Mfano:
  ''Jina lako ni nani?'' Mwalimu aliuliza – Mwalimu alitaka kujua jina lake.
- Nafsi katika msemo wa taarifa hubadilika k.m
  Mimi – yeye .          Sisi – wao.
- Wakati hubadilika k.m –Sasa – wakati huo – me – alikuwa.
  - ta / ki – nge          - leo – siku hiyo.
- Mahali pia hubadilika mfano
  – Hapo – hapo          - Huku – kule
  - Leo jioni – jioni hiyo          - Kwetu – kwao.
- Neno huwa yakuwa ; ya kwamba ; hutumiwa kutangulisha usemi wa taarifa .
- Mara nyingi wakati huwa kutoka wakati uliopita.

**ZOEZI**

**Badilisha sentensi zifuatazo kulingana na maagizo yaliyo mabanoni.**

1. "Nitaenda kwangu leo joini," Joshwa alisema. (taarifa)
2. Julius aliuliza,"Unaitwa nani?" (taarifa)

3. Zakaria alisema kuwa angekuwa tajiri angenunua gari. (Halisi)
4. Mwalimu Monyoro alitaka kujua mahali nilikuwa aliponiita. (Halisi)
5. Tereza alimaka kuwa mvua ingenyesha siku hiyo jioni. (Halisi)

## UKUBWA NA UDOGO WA MAJINA YA KISWAHILI

- Baadhi ya majina ya Kiswahili huweza kuwekwa katika matawi matatu kulingana na vimo. Huweza kuwa katika udogo, wastani na ukubwa.
- Majina katika udogo huonyesha vitu vilivyo katika kimo cha chini ikilinganishwa na hali ya kawaida.
- Maneno katika tawi hili pia huonyesha mabezo / madharua; huwa kinachozungumziwa kinadharauliwa k.m Hiki ndicho kigari chako.
- Maneno katika tawi la tatu huonyesha kuwa kitu kinapatikana katika kimo cha juu kuliko hali ya kawaida.
- Vilevile huonyesha madharau / maudhiko k.m Toto lile lina tabia mbaya sana.
- Kijisiwa huwa udogo ikilinganishwa na kisiwa.

**Mifano**

| Kawaida | Udogo | Ukubwa |
|---|---|---|
| Ngo'mbe | Kigombe | Gombe / Jigombe |
| Ndege | Kidege | Dege / Jidege |
| Panda | Kijipanda | Jibanda |
| Nyoka | Kijoka | Joka/ Jijoka |
| Mbuzi | Kibuzi | Buzi/ Jibuzi |
| Mbwa | Kijibwa | Jibwa |
| Kiuno | Kiiuno | Jiuno |
| Goti | Kijigoti | Jigoti |
| Kikapu | Kijikapu | Kapu/ Jikapu |
| Mdudu | Kidudu | Jidudu / Dudu |
| Saa | Kijisaa | Jisaa |
| Mkono | Kikono | Jikono / Kono |
| Sinia | Kijisinia | Jisinia |
| Barua | Kijibarua | Jibarua |
| Mto | Kijito | Jito |
| Mlima | Kilima | Jilima / lima |
| Mtungi | Kitungi | Jitungi |
| Kisiwa | Kijisiwa | Jisiwa |
| Kitanda | Kijitanda | Jitanda |
| Mwana | Kijana | Jana |
| Mwanamwali | Kijanajali | Janajali |

- Majina yanayoanza na "ji" huongezewa " ji" k.m Jiwe – Jijiwe
  - Jicho – jijicho
- Majina yanayoanza kwa "mwa" hupachikwa "ji" mwanzoni badala ya mwa k.m
  - Mwanamke – janajike
  - Mwanadamu – janadamu
- Majina yaliyo na mwanzo maalum hupachikwa "ji" mwanzoni k.m
  - Kofia - jikofia
  - Karatasi – jikaratasi
- Majina yasiyokubali kuondolewa "ki" hupachikwa "ji" k.m
  - Kiti – jikiti
- Majina yanayoanza na "ki" huwekwa "ji" (sio yote yanayokubali ) k.m
  - Kiatu – jiatu
- Majina yaanzayo kwa "m" ikiwa inatamkwa pekee .m. huondolewa k.m
  - Mkoba – koba
  - Mkono – kono
- Majina yeye silabi mbili ambazo hutamkwa zote huondolewa herufi ya kwanza (k.m na ng, nd, ny, mb)k.m
  - Ndama – dama
  - Njugu – jugu
  - Ndizi – dizi
  - Ngombe – gombe
- Majina yaanzayo kwa **u** huwekwa **j** na kuondoa **u** k.m
  - Uzi – juzi
  - Ukuta – jikuta
  - Ubao – jibao
- Majina yaanzayo na **ch** huwekwa **j** k.m
  - Chombo – jombo
  - Chuma – juma
  - Choo – joo

**KUMB:** Ukitaka kupata udogo sema ukubwa + ki = udogo
**Mfano:** Jembe +ki = kijembe.
Gombe + ki = kigombe.

## ZOEZI

Badilisha sentensi zifuatazo katika:
(i) Wingi
(ii) Udogo katika umoja
(iii) Udogo katika wingi
(iv) Ukubwa katika umoja
(v) Ukubwa katika wingi

1. Mtoto huyu ana tabia mbaya.
2. Ng'ombe wangu amevunjika mguu.
3. Dawati lake limevunjikavunjika.
4. Mwanamke alitishwa na nyoka mtoni.
5. Jiji hili ni kubwa jiji lolote.

## TASHBIHI / TASHBIHA

- Tashbihi ni hali ya kufananisha kitu na kingine / hali na nyingine. Maneno kama, mithili ya, falau, sawasawa na, hutumika kufananisha.

1. Mzuri kama malaika.
2. Zito kama nanga.
3. Mlevi kama komba.
4. Asema sana kama chiriku.
5. Mwenye bidii kama mchwa.
6. Mzima kama kigongo ama ngarange ya mvule.
7. Msiri kama usiku / kaburi / kobe.
8. Kujitia katikati kama mchuzi wa ugali.
9. Mporokaji kama mlevi.
10. Mwoga kama kunguru.
11. Nata kama gundi.

12. Mwenye wivukam mke mwenza.
13. Ganda kama kigaga.
14. Pukutika kama majani ya mti.
15. Kumganda mtu kama kupe.
16. Nywele nyingi kama singa.
17. Laini kama hariri / pamba.
18. Mvumilivu kama mtumwa.
19. Tamu kama asali.
20. Adhibiwa kijeshi.
21. Mrefu kama ngamia komanzi / twiga / mlingoti.
22. Pana kama uwanja wa ahera.
23. Mwembamba kama ufito / uzi.
24. Tamu kama asali / halua.
25. Mkaidi kama punda / kihongwe.
26. Asi kama nunda / pakashume.
27. Kuadimika kama maziwa ya kuku.
28. Shingo kama upanga.
29. Kali kama wembe / pilipilihoho.
30. Ngara kama mwezi.
31. Maringo kama chongoo.
32. Maridadi kama mbega.
33. Hakika kama mauti.
34. Nguruma kama radi / simba.
35. Fupi kama nyundo / mbilikimo.
36. Mjinga kama samaki / kondoo.
37. Tumbo kama kiriba.
38. Haraka kama umeme.
39. Epesi kama usufi.
40. Julikana kama pesa.
41. Nuka kama kidonda / beberu / mzoga.
42. Kulandana kama maziwa na tui.
43. Konda kama ng'onda.
44. Nyooka twaa kama mwanzi.
45. Baidika kama ardhi na mbingu.
46. Joto kama tanuri.
47. Chungu kama shubiri.
48. Paa kama moshi.
49. Ekundu kama damu.
50. Mnene tibwatibwa kama hanziri.
51. Pofu kama jongoo.
52. Fuatana kama kumbikumbi.
53. Lazima kama ibada.
54. Mzembe kama kupe / chaza.
55. Hakika kama mauti.
56. Kigeugeu kama kinyonga / lumbwi.
57. Mweusi kama mpingo / makaa / lami / kaniki mashizi.
58. Mwaminifu kama njiwa.
59. Mnafiki kama panya / ndumakuwili.
60. Huzuni kama mfiwa.
61. Safi kama mfua uji.
62. Nadra kama kinyesi cha samaki.
63. Wazi kama mchana.
64. Tetemeka kama saa kweche.
65. Tengana kama ardhi na mbingu.
66. Shirikiana kama mpini na jembe.
67. Kinyume kama tumbo na mgongo.
68. Kutoelewana kama maji na mafuta.
69. Tofauti kama moto na barafu.
70. Kutoaminiana kama kuku na mwewe.
71. Sauti nzuri kama kinanda.
72. Fanana kama shilingi kwa ya pili.
73. Msahaulifu kama nyati.
74. Imara kama chuma ya pua.
75. Bahati kama mtende.

**VIKEMBE**

- Vikembe ni vitoto / vizawa vya viumbe mbalimbali.

| Mnyama | Kikembe |
|---|---|
| Ng'ombe | Ndama |
| Nguruwe | Kiguruwe / kivinimbi |
| Ndege | Kinda |
| Punda | Kihongwe |
| Simba | Shibli / kibuai |
| Paka | Kipusi / kinyaunyau |
| Sungura | Kituju / kitungule |
| Mbwa | kilebu / kidue / kijibwa |
| Nyuki | Jana |
| Bata | Kiyoyo |
| Papa | Kinengwe |
| Nyoka | Kinyemere |
| Kipepeo | Kiwavi |
| Tai | Kikangazi |
| Nyani | Kigunge |
| Ngamia | Nirihi |
| Kuku | Kifaranga |
| Farasi | Kitekli |
| Chui | kisui / chongole |
| Ndovu | Kidanga |
| Mamba | Kingwena |
| Fisi | Kikuto / bakaya |
| Farasi na punda | Nyumbu |
| Mdudu | King'onyo |
| Nzi | Buu / kiluwiluwi |
| Nyangumi | Chengo / kinyangunya |
| Nge | Kisuse |
| Kondoo | Kibebe / katama/ mwanakondo |
| Mbu | Kiluwiluwi |
| Nzige | Kimatu / tunutu / funutu / maige |
| Mbweha | Nyamawa |
| Mbuzi | Kimeme / kibuli / tangina / mwanambuzi |
| Chungu | Kwida |

**MAJINA YA MAKUNDI**

| | |
|---|---|
| • Hadhara ya watu | • Thurea ya nyota |
| • Hukumu ya watu | • Mlolongo wa magari |
| • Halaiki ya watu | • Kipeto cha barua |
| • Sisisi ya watu | • Maktaba ya filamu |
| • Hombo la samaki | • Kicha cha funguo / mboga |
| • Mtungo wa samaki | • Kipeto cha mpunga / mtama |
| • Numbi ya samaki | • Chane ya ndizi |
| • Funda la maji | • Mkungu wa ndizi |
| • Tone la maji | • Shungi la nywele |
| • Kidimbwi cha maji | • Tita la kuni / nguo |
| • Tama la maji | • Kikundi cha waimbaji |
| • Karne ya miaka | • Kikoa cha wachezaji |
| • Doti ya kanga / leso | • Tano ya chokaa |
| • Jopo la majaji | • Kambi ya wanajeshi |
| • Tonge la ugali | • Shumbi la udongo |
| • Fala la pishi | • Safu ya milima |
| • Biwi la takataka | • Kambi ya wakimbizi |
| • Korija la vitambaa | • Halmashauli ya shula / mitaa |
| • Mzengwe wa waasi | • Tanuu ya makaa |
| • Koja la maua | • Kipini cha dhahabu |

| | |
|---|---|
| • Bumba la nyuki | • Nakidi ya pesa |
| • Kidani cha almasi | • Jozi ya viatu |
| • Gora ya leso | • Robota la ngozi |
| • Msitu wa miti | • Kikataa cha shamba |
| • Sharafa la ndefu | • Manyunyu ya mvua |
| • Minofu ya nyama | • Kamati ya uchunguzi |
| • Wingu la moto | • Kichala cha matunda |
| • Cheche za moto / matusi | • Kifurushi cha kalamu |
| • Jora ya bafta / vitenge | |

## TANAKALI ZA SAUTI

| | |
|---|---|
| 1. Maji yalimwagika mwaa! | 36. Kufa fofofo / foo! |
| 2. Kuvuma vum! | 37. Kupukutika machozi kupukupu! |
| 3. Tawi lilianguka chini kach! | 38.Kuteketea teke teke! |
| 4. Kuvunjika kacha! | 39.Kusukumwa marshimarshi! |
| 5. Jiwe lilianguka kwenye tope kach! | 40.Kufyatuka fyatu fyatu! |
| 6. Mbwa alibweka bwe! Bwe! Bwe! | 41.Kuponea chupuchupu/ almanusura! |
| 7. Anguka mchangani tifu! | 42.Kufurika furi furi! |
| 8. Giza totoro! | 43.Mkonde tu kimbaumbau! |
| 9. Sarafu ilianguka mchangani tifu! | 44.Kuchemka chem chem! |
| 10. Zubaa zubezube! | 45.Mnene tibwatibwa! |
| 11. Tega sikio ndi! | 46.Kukoroma rororo/korr! |
| 12. Kukauka kaukau! | 47.Funika gubigubi/ kubikubi! |
| 13. Kudidimia di di di! | 48. Nga'nga'na nga'nga'nu nga'nga'nu! |
| 14. Kohoa kokoko! | 49. Mulika mwaa! |
| 15. Kubingirika bingiri bingiri! | 50. Kuchukuliwa juu hangahanga! |
| 16. Kupasuka paa! | 51. Kulewa chakari / leuleubin chopi! |
| 17. Kuchefua chefu chefu! | 52. Kujaa chomboni pomoni! |
| 18. Kuvunjika vurugu vurugu! | 53. Kulowa chapachapa / chepechepe! |
| 19. Eupe pe! Pe! Pe! | 54. Kukamata papatu! |
| 20. Radi ilipiga papapa! | 55. Kuzimia zii! |
| 21. Eusi ti! | 56. Kupambana kukuru kakara! |
| 22. Saa ilisikika tiktak! | 57. Kunyooka twaa! |
| 23. Mulika mwa! | 58. Kupelekwa mkikimkiki! |
| 24. Kubunga ngaa! | 59. Kupamba pambe pambe! |
| 25. Funga mizigo ndi! | 60. Kubebwa hobelahobela! |
| 26. Kuduwaa waa! | 61. Kutiririka tiriri |
| 27. Gonga ngo! Ngo! Ngo! | 62. Kunga'nga'nia kukutu! |
| 28. Elewa fika! | 63. Nukia nhh! |
| 29. Kulipuka pu! | 64. Kutumbukia tumbwi! |
| 30. Kupuliza puu! | 65. Penya fya! |
| 31. Kutwanga twaa! | 66. Kula fyuu! |
| 32. Shiba ndi! | 67. Nuka fee / mff! |
| 33. Kuteleza parr! | 68. Kuchemka chemchem! |
| 34. Kutafuna tafutafu! | 69. Kubwatika bwata! |
| 35. Kunyamaza zii! / Ji! | |

## USHAIRI

- Anayetunga mashairi – malenga.
- Anayeimba na kukariri mashairi – mghani.
- Anayetunga na kuimba nyimbo na mashairi – manju.

## AINA ZA MASHAIRI

1. Shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti - tathnia (uwili)
2. Shairi lenye mishororo mitatu katika kila ubeti - tathlita (utatu)
3. Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti - tarbia (unne)
4. Shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti - takhmisa (utano)
5. Shairi lenye mishororo sita katika kila ubeti - taslita (usita)
6. Shairi leye mshororo mmoja - Tathmina

### Sehemu katika shairi

(a) **UBETI** - Ni kifungu kimoja cha shairi na huundwa kutokana na idadi ya mishoro.
(b) **UKWAPI** - Ni kipande cha kwanza cha mishororo.
(c) **UTAO** – Kipande cha pili cha mshororo.
(d) **MWANDAMIZI** – Mshororo wa nne katika ubeti.
(e) **MWANZO** – Mshororo wa kwanza katika ubeti.
(f) **MLOTO** – Mshororo wa pili katika ubeti.
(g) **MLEO** – Mwanzo wa tatu katika ubeti.
(h) **KIBWAGIZO** – Mwanzo wa nne katika ubeti.
(i) **MIZANI** – Ni silabi katika msitari wa ubeti k.m
U – be- ti - mizani 3, Monyoro – Mo – nyo – ro
(j) **VINA** – Ni silabi za maana moja / zenye matamshi mamoja inayopatikana mwishoni au katikati mwa mshororo.
(k) **MKARAGUNI** – Ni shairi ambalo kila ubeti una vina tofauti.
(l) **KIKWAMBA** – Kila ubeti huanza kwa neno moja.
(m) **NGONJERA / MARUMBANO** – Ni majibizano / majadiliano kati ya watu wawili.
(n) **TABDILA** – Kubadili irabu / vokali kama dunia – duniya.
(o) **MAZIDA** – Kuongeza silabi katika jina bila kupoteza maana yake asili ya neno lenyewe k.m Mwengine_ mwenginewe.
(v) **INKISARI** – Kufupisha k.m Sikasiri – sikasiriki n.k.
(q) **MSUKO** – Kibwagizo kuwa kifupi kuliko mshororo.
(r) **LAKABU** – Silo jina halisi la mshairi bali lile analojibandika.
(s) **UTENZI** – Mashairi juu ya mtu mausio dini n.k

## NYAKATI ZA SIKU

(i) Mapambazuko / macheo / mawio – Kunakucha ili kuanze siku mpya – Alfajiri.
(ii) Majogoo kwenye saa tisa – alfajiri kuu.
(iii) Saa kumi na saa kumi na moja alfajiri – Alfajiri mbichi.
(iv) Baada ya alfajiri / mafungulia ngombe – Asubuhi.

(v) Katikati ya mchana, wakati wa jua la utosi / wakati wa mtikati – Adhuhuri.
(vi) Kipindi cha kuanzia saa moja hadi saa tatu usiku – Isha.

**MISIMU**

(i) **Kiangazi** - Kipindi cha mwaka chenye jua kali na joto jingi chari. Huwapo baina ya vuli na masika.
(ii) **Masika** - (kifuku) – Kipindi cha joto na mvua nyingi.
(iii) **Kipupwe** – Kipindi cha baridi kali.
(iv) **Mchoo** – Majira ya mvua ndogondogo kati ya Julai na oktoba.
(v) **Kaskazi** – Msimu wa upepo unavuma kutoka Kaskazini Mashariki na wenye joto kali hasa katika uwanda wa pwani.
(vi) **Vuli** – Kipindi cha mvua fupi ziletwazo na upepo wa Kaskazini.
(vii) **Yahom** – pepo za Magharibi.
(viii) **Kusi** - pepo za Kusini.
(ix) **Matlai** – pepo za Mashariki.
(x) **Kaskazi** – pepo za Kaskazini.

**SAUTI NA MILIO YA VIUMBE NA VITU**

- Ngombe – Kukoroma / mroromo.
- Mbwa – Kubweka / mbweko.
- Simba – Kunguruma / mgurumo.
- Chui – Mvumo / kuvuma.
- Nyoka – Huluza / muluzo.
- Tembo – Kutetea / mteteo / hukokoroka.
- Upepo – kuvuma / mvumo
- Moto – Kurindima / mrindimo.
- Nyasi kavu zinazoteketea – Hutatarika / mtatariko.
- Chungu jikoni – Hutokota / mtokoto.
- Mkanyago wa majani makavu – Mchakacho / parakacha.
- Kuongea lugha isiyoeleweka – Kukorokocha / mkorokocho.
- Sauti ya kusitasita – Kugugumiza.
- Mlio wa ngoma – Mdundo.
- Sauti ya bomu / kombora – Mlipuko.
- Sauti ya bunduki, bastola/ risasi – Mfyatuko.
- Kutoa sauti usingizini unapoota – Kuhohosa / kuweweseka / mweweseko.
- Kuutoa pumzi kwa nguvu – Kutweta / kuhema.
- Kusema maneno ya matusi – Kupyora / upyoro.
- Kupiga piga mbawa – Kupapatika / mpapatiko.
- Ng'ombe hucheuwa na panya huguguna.
- Nyoka hutambaa na jongoo hunyiririka.
- Sauti ya mtu aliye usingizini kukoroma / mkoromo / huforota / hukorota.
- Mlio wa hatari wa meli vitani jeshini – kingora.
- Mlio mkali wa hofu kana kwamba unateswa – unyende / kite.
- Nyuki – Michato.
- Mbu - husikizia
- Kondoo – hugogurura / humemea
- Farasi – hutekera.
- Nyuni – hukorokocha.
- Miti – hutukutika wakati wa upepo.
- Kengele – Hukiliza.
- Saa – Hutukitika.
- Kitheme – hukimiza.
- Mlevi – Huboboja maneno.
- Fisi – Hututusa.
- Tembe – Hutetea / hutora.
- Mtu – Hulalama maudhini.
- Kitata – Kigugumizi.
- Mchawi – Hurongonya.
- Punda_-_ kupukira

**MAJINA YA MIEZI KWA KISWAHILI.**

| | |
|---|---|
| • January – Januari | • July - Julai |
| • February – Februari | • August - Agosti |
| • March – Machi | • September - Septemba |
| • April – Aprili | • November - Novemba |
| • May – Mei | • October - Oktoba |
| • June – Juni | • December - Desemba |

Juzi, Jana, Leo, Kesho, Keshokutwa, Mtondo-mtondogoo, kitondo – kitondogoo.
Leo,jana, juzi,majuzi, fuzijuzi, kitojo, kijomba.

**MSAMIATI WA RANGI.**

- Eupe – White.
- Samawati – Blue.
- Eusi – Black.
- Kijani kibichi – Green.
- Ekundu – Red.
- Urujuani – Violet.
- Zambarau – purple.
- Zarafani / Manjano – Yellow.
- Hudhurungi – Brown.
- Kijivu – Grey.
- Kahawia – Brown.
- Nili – Indigo(dark blue)
- Light Green – Binti marembo.
- Golden – Zari.
- Silver – Fedha.
- Colourless – sorangi.

**MADINI**

| | |
|---|---|
| • Gold – Dhahabu | • Copper – shaba nyekundu |
| • Johari – zinki | |
| • Diamond – Almasi | • Chumvi – chokaa ya mawe |
| • Zumaridi – Bati | • Precious stones – Vito |
| • Silver – Flouspar | • Jasi – Chuma cha pua |
| • Magadi – Jasi | • Feleji – Matale/ itale |
| • Lead – Risasi | • Tanzanaita – Ulanga |
| • Iron – chuma | • Oil – Mafuta |
| • Pearls – Lulu | • Asbesto – Yakuti |

**MAPAMBO YA MWILI**

**MASIKIONI**

- Jaribosi, Herini, Bali, Kipuli, Pingo

**KICHWANI**

- Pini, Kitana, Kibanio cha nywele, Taji, Shali,

Hina, Mafuta, Kikuba

**PUANI**

- Kishaufu, Hazama, Kikero, Kipini, Shemere

**KIFUANI**

- Mkufu, Kidani, Nishani, Tondoti, Nyota za nyadhifa mbalimbali

**SHINGONI**

- Mkufu, Shanga, Kigwe, Useja, Wanja, Koa, Kiganja, Kidani, Kikuba, Nishani, Tai, Ushanga

**MIGUUNI**

- Njuga, Kipingo, Nyerere, Furungu, Kigezi, Kikuku, Wanja, Kekee, Timbi, Udodi, Hina, Milia

**MIKONONI**

- Bangili, Pete, Hina, Wanja, Usinga, Nembo, Kikuku, Kekee, Pochi, Pingu

**USONI**

- Chale, Nembo, Taruma, Ndonya, Jebu, Ukaya, Kigwe,

**KIUNONI**

- Masombo / Kibwebwe, Mshipi, Kogo, Malindi, Kondavi

## MAGONJWA

- Tauni – (plague) - uele wa homa kali unaosababishwa na viroboto wa panya.
- Malale – (Sleeping sickness) – ukosefu wa usingizi,Unaambukizwa na mbu
- Tetewanga – (Chicken pox) – Mapele yanayoambatana na homa kali.
- Suma – (Measles) – Surua / ukambi.Ngozi huwa na vipele hasa kwa watoto.
- Ndui – (Small pox) – Pele nyingi zenye maji na usaha.
- Ukoma – (Leprosy) – Kukatika viungo vya mwili.
- Kifafa – (Epilepsi) – Ni ugonjwa wa kupoteza fahamu.
- Kipindupindu / waba– (Cholera) – kuhara na kutapika sana.
- Kaswende / Seneneko (siphylis) –ugojwa wa zinaa ambapo mtu hujibuka sehemu za siri.
- Kifua kikuu – (Tuberculosis) – kukohoa sana, kifua hulia unapokohoa.
- Pepopunda – (Tetanus) – ugonjwa unaosababishwa na vifaa vilivyoshikwa na kutu.
- Homa ya matumbo – (Typhoid) –
- Homa iletwayo na mbu aitwaye anofelesi–(Malaria) –
- Kichocho - (Bilhazia) – kukojoa damu,husababishwa na vidudu vya konokono.
- Kuhara – (Diarrhoea) –
- Kupooza – (Polio) – ugojwa wa mishipa katika uti wa mgongo unaosababisha kupooza kwa viungo.
- Sotoka – (Rinderpest) – ugonjwa unaoshambulia mifugo.
- Homa iletwayo na chawa – (Typhius) –
- Saratani – (Kansa) Cancer – ni ukuaji usio wa kawaida wa seli katika mwili.
- Kimeta – (Anthrax)___ugonjwa uvamiao mifugo.
- Matende – (Elephantiasis) – Kuvimba miguu.
- Utapia mlo –(marasmus) -_ni ugonjwa unaosababishwa na ukosefu wa chakula.
- Kifaduro - (Diptheria) –
- Manjano - (Yellow fever) –
- Kupooza - (paralysis) –
- Nyongoa – (Rickets) –
- Safira – (anaemia) –
- Machumbwi – (Mumps) –kuvimba mashavu hadi chini ya taya.
- Choa – (Ringworms)
- Lalab – (Rabies)
- Jibu – (Abscess)
- Pumu – (Asthma)
- Pele – (Scabies)

## MAVAZI

| | |
|---|---|
| 1. Rinda – | 16. Makubazi – |
| 2. Shimizi /gaghuro– | 17. Kitema – |
| 3. Kocho / Chupi – | 18. Blauzi – |
| 4. Tai – | 19. Seruni – |
| 5. Kanchiri / sidiria – | 20. Kaniki – |
| 6. Kaptura / bombo– | 21. Shati – |
| 7. Kaputi – | 22. Suruali – |
| 8. Surupwenye / Bwelasuti | 23. Mahazamu – |
| 9. Kofia – | 25. Uwinda - |
| 10. Bargashia / Bulibuli | 26. Malapa – |
| 11. Koti – | 27. Njuti – |
| 12. Fulana – | 28. Masombo – |
| 13. Shali – | 28. Kitenge – |
| 14. Buibui – | 29. Kanga – |
| 15. Kitambi – | 30. Kisutu – |

**MSAMIATI / MAJINA YA UKOO / NASABA**

1. Mzazi wa kiume– Baba / abu.
2. Mzazi wa kike – Mama / nina.
3. Ndugu wa kiume – Kaka.
4. Ndugu wa kike – Dada.
5. Mtoto wako uliyemzaa – Mwana.
6. Mtoto wa mwanao – Mjukuu.
7. Mtoto wa mjukuu – Kitukuu.
8. Mtoto wa kitukuu – Kilembwe.
9. Mtoto wa kilembwe – Kilembwekeza / Kining'ina.
10. Mzazi wa kiume wa babangu / mamangu – Babu.
11. Mzazi wa kike wa babangu / mamangu – Nyanya / Bibi.
12. Dada na kaka huitana – Umbu.
13. Mtoto wa kaka / dada huitwa – Mpwa.
14. Kaka wa baba yako huitwa – Ami / amu / baba mkubwa / mdogo.
15. Kaka wa mama yako – Mjomba / hau.
16. Dada wa baba yako – Shangazi / mbiomba / amati.